1013/ 2
PI KISWAHILI
KARATASI YA 2
MWIGO
MACHI 2019
Muda: Saa 3

# FASIHI NA MBINU ZA KUFUNDISHIA

Saa 3

*Maagizo*
*a) Karatasi hii ina sehemu mbili kuu FASIHI na MBINU ZA KUFUNDISHIA.*
*b) Jibu maswali MATATU katika sehemu ya Fasihi. Swali la USHAIRI na TAMTHILIA ni la LAZIMA.Kisha chagua swali moja kutoka RIWAYA au HADITHI FUPI. Usijibu maswali mawili kutoka kwa kitabu kimoja. Maswali yote katika sehemu ya MBINU ZA KUFUNDISHIA ni ya LAZIMA.*
*c) Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

Kwa matumizi ya mtahini pekee.

| Sehemu | Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|---|
| A | 1 | 15 | |
| | 2a | 15 | |
| | 2b | 15 | |
| | 3a | 15 | |
| | 3b | 15 | |
| | 4a | 15 | |
| | 4b | 15 | |
| B | 5 | 18 | |
| | 6 | 17 | |
| | 7 | 20 | |
| | Jumla | 100 | |

Karatasi hii ina kurasa 14 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba maswali yote yamo

## SEHEMU A: FASIHI (AL. 45)

1. USHAIRI
*Miali ya Ushairi* : PI Iribemwangi n Kevin Wamalwa
Soma shairi hili kisha ujibu maswali.

**SUBIRA**

Subira hulka adimu, kwa mja mtaka heri,
Hali iwapo ngumu, ni faradhi kusubiri,
Kwa kila lako jukumu, kalitende kwa subira,
Subira mja wa kheri, subira huvuta heri.

Mambo tenda mosimosi, hili likisha na hili,
Mwenye pupa katu hesi, kufutu kula shubiri,
Ni mja wa wasiwasi,anahaha na hatuli,
Mwangata mbili fahamu, mbambo mwenga hwengaenga.

Sikate tamaa mbuye, iwa' ni pole mwendo,
Ahitimuye si yeye, mwenye papara vitendo,
Ni yule asubiriye, asiyependa vishindo,
Bandu bandu hwisha gogo, na chururu si ndo ndo ndo.

Maisha ni ya vidato, yaanze na uliko,
Huanze tete ja mtoto, pasi nazo papariko,
Zitue mpwitompwito, za kwenda huko na huko,
Uwapo wa kuvuka mto, ngoja fikiye ivuko.

Ukidai ngojangoja , huja kuumiza tumbo,
Eti subra si haja, kataka parama mambo,
Kutaka kukidhi haja, haja za kutuza tumbo,
Uli mja pupa nawe, hudiriki kula tamu.

Sitake makubwa nawe, yasiyo ya kufu yako,
Ukijipa na kiwewe, nashanina hamaniko,
Ukihofu sichelewe, tajitia sikitiko,
Mbona hukumbuki mja, jikune ujipatapo?
(Kevin Wamalwa)

**Maswali**

a) Eleza wosia wa mshairi kwa msomaji (al.4).
b) Taja bahari ya shairi hili kwa mujibu wa kituo  (al.2).
c) Bainisha upungufu unaojitokeza katika shairi hili (al. 2)
d) Kwa kutoa mifano onyesha namna mwandishi alivyotumia mbinu hizi (al.3)
i) Inkisari.
ii) kufinyanga sarufi.
iii) Deheni
e) Taja methali mbili zinazokinzana katika shairi hili (al.2).
f) Andika ubeti wa nne katika lugha nathari (al.2).

## 2. TAMTHILIA

*Upepo wa Mvua*: Jeff Mandila

Jibu swali la 2a au 2b

**(a).** "wananchi , jinsi mnavyojua, tunastahili kudumisha amani na usalama katika vijiji vyetu. Kulingana na kanuni za serikali yetu tukufu, mtu akipatikana amevuruga usalama, ni sharti aadhibiwe.."

i) Eleza muktadha wa dondoo hili (al.4).
ii) Mazungumzo haya ni kinaya. Thibitisha (al.6).
iii) Eleza sifa tano za msemaji (al.5).

**(b).**

i) Onyesha changamoto zinazowakumba wakaaji wa Bondeni katika juhudi za kupambana na uongozi dhalimu wa Chifu Mtoro (al.6).
ii) Eleza namna mwandishi alivyoangazia maudhui ya elimu katika tamthilia ya *Upepo wa Mvua* (al.6).
iii) Eleza mbinu ya sadfa kama inavyobainika katika tamthilia (al.3).

## 3. RIWAYA

*Pendo La Karaha*: John Habwe

Jibu swali la 3a au 3b

**(a**) i) Mwandishi ameangazia umaskini na matokeo yake katika jamii katika riwaya ya *Pendo la Karaha*. Eleza (al.10).
ii) Kwa mujibu wa riwaya, Eleza juhudi za serikali katika kupambana na changamoto zinazowakumba vijana (al.5).

**(b)**

" Kama bosi wake alivyomweleza kuwa angependa uhusiano ule uwe siri, kila mmoja wao alijitahidi kuihifadhi siri...."

i) Eleza muktadha wa dondoo hili (al.3).
ii) Mazungumzo haya yanadhihirisha uozo uliojikita katika jamii hii. Kwa kutumia mifano zaidi toa maelezo kuthibitisha kauli hii (al. 8).
iii) Eleza sifa za mrejelewa (al.4).

**4. HADITHI FUPI**

*Vazi La Mhudumu Na Hadithi Nyinginezo* : P.I. Iribemwangi na Hamisi Babusa (Wahariri)

**(a)**

i) Onyesha namna vazi la Mhudumu Daudi linavyochangia katika matukio yanayobainika katika hadithi ya *Vazi la Mhudumu* (al.6).

ii) Dhihirisha namna ukosefu wa maadili unavyobainika katika hadithi ya *Vazi la Mhudumu* (al. 6).

iii) Eleza namna mwandishi wa hadithi hii alivyotumia mbinu ya sadfa (al.3).

**(b)**

i) Onyesha namna mwandishi alivyoangazia maudhui yafuatayo katika hadithi ya *Lucia Mtoto wa Mama*.

a) Malezi (al.5)

b) Taasubi za kiume (al.4).

ii) Eleza sifa za Lucia kama inavyobainika katika hadithi ya *Lucia Mtoto wa Mama* (al.6).

**SEHEMU B: MBINU ZA KUFUNDISHIA (AL.55)**

***Jibu Maswali YOTE katika sehemu hii***

5. Unajiandaa kufundisha insha ya kubuni katika darasa la tano.
a) Eleza mambo manne muhimu utakayowaelekeza wanafunzi kuhusu uandishi wa insha hii (al.8).
b) Eleza changamoto ambazo wanafunzi hukabiliana nazo katika uandishi wa insha kama hii (al.5).

c) Eleza manufaa ya somo la insha kwa wanafunzi (al.5).

6. Unanuia kuandaa ratiba ya Kiswahili kwa darasa la nne.
a) Taja vifaa vinne ambavyo utahitaji kwa shughuli hii (al.4).
b) Eleza mambo matano utakayozingatia katika kuandaa ratiba hiyo (al.5).

c) Eleza manufaa ya sehemu hizi katika andao la somo
i) Utangulizi (al. 2).

ii) Tathmini nafsia (al.3).

d) Taja umuhimu wa mwalimu kutumia vifaa halisi kwa vipindi vya Kiswahili (al.3).

7. a) Eleza namna utakavyotumia mbinu ya ziara za kimasomo katika kufundisha msamiati wa viwandani kwa darasa la saba (al.12).

b) Eleza manufaa ya kuwafundisha wanafunzi vipindi vya kusikiliza na kuongea (al.8).